
# Women on Waves: Kujifungua Kwa Njia Ya Usalama Ukitumia Misoprostol


**Misoprostol yaweza kuzuia kupoteza damu kwa wingi ukeni baada ya kujifungua, kwa lugha ya kimombo, ( postpartum hemorrhage).**
**Hivi ndivyo unavyoweza kuitumia kwa njia ya usalama.**

www.womenonwaves.org
www.womenonweb.org




**1.**
**Mara tu baada ya kujifungua:**
Mkaushe mtoto kisha mlaze juu ya tumbo la mama. Funika mtoto kwa nguo ya joto au blangeti.

**2.**
**Ndani ya dakika MOJA baada ya mtoto kuzaliwa**:
Papasa tumbo ili kukagua kama hakuna mtoto mwingine, yaani mapacha.




**3.**
**Ndani ya dakika MOJA baada ya mtoto kuzaliwa:**
Weka vidonge vitatu vya Misoprostol (kila tembe moja 200mcg) chini ya ulimi wa mama aliyejifungua ili kuleta machungu. Ziwache zitulie angalau kwa nusu saa kabla ya kuzimeza.





---

**4.**
**Dakika tatu baada ya kujifungua:**
Funga kamba ya kitovu ukitumia nyuzi mbili safi kabla ya kukata kamba ya kitovu ukitumia wembe mpya na ngojea mfuko wa mimba kutoka.



**5.**
**Baada ya mfuko wa mimba kutoka:**
Kanda tumbo kuanzia juu baada ya mfuko wa mimba kutoka hadi tumbo lirudi kuwa kama mpira mgumu. Fanya hivi kila baada ya dakika 15 kwa kipindi cha masaa mawili yanayofuata.



## NENDA HOSPITALINI KWA HARAKA KAMA:

Mfuko wa mimba haujatoka ndani ya dakika 30

**au**

Mwanamke kuanza au kuendelea kutokwa na damu nyingi baada ya kutumia Misoprostol

**Kwa taarifa zaidi, nenda kwa www.womenonwaves.org au tuma barua pepe kwa info@womenonweb.org**

Picha zimetolewa kwa hisani ya Hesperian